

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-22-2114512, 2116898

E-mail: [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)

Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)

Faksi: 255-22-2113425



OFISI YA RAIS,

IKULU,

1 BARABARA YA BARACK OBAMA,

11400 DAR ES SALAAM.

Tanzania.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli leo tarehe 06 Mei, 2018 ameendelea na ziara yake Mkoani Morogoro ambapo amefungua kituo bora cha mabasi cha Msamvu kilichopo katika Manispaa ya Morogoro.

Kituo hicho kimejengwa kwa ubia wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro yenye hisa asilimia 40 na Mfuko wa Pensheni wa LAPF wenye asilimia 60 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 12, na uendeshaji wake umewekwa chini ya kampuni iitwayo Msamvu Properties Company (T) Limited inayojiendesha kibiashara.

Mkurugenzi Mkuu wa LAPF Bw. Eliud Sanga amesema kituo hicho kimejengwa kwa kuzingatia mahitaji muhimu yakiwemo maeneo ya maegesho ya mabasi 110, magari madogo 68, pikipiki 50, kituo cha polisi na ukaguzi wa mabasi, maduka makubwa 26, vibanda vya biashara 19, ofisi za tiketi 40, migahawa ya chakula 5, vyoo 70, benki, ofisi, jengo la utawala na kimewekewa mifumo ya usalama (CCTV), matangazo na ukumbi wa mikutano.

Bw. Sanga amesema licha ya kuboresha huduma za usafiri wa abiria, katika mwaka uliopita kituo hicho kimefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka Shilingi 350,000 kwa siku hadi kufikia Shilingi 3,000,000 kwa siku.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*) Mhe. Selemani Jafo amshukuru Mhe. Rais Magufuli kwa Wizara yake kutengewa Shilingi Bilioni 146 za miradi mbalimbali, ambapo kati yake Shilingi Bilioni 67.3 ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mabasi 8 hapa nchini kikiwemo kituo cha mabasi cha Dar es Salaam kilichotengewa Shilingi Bilioni 50.9 na amebainisha kuwa vingine 7 vitajengwa kwa kutumia fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia.

Nae Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajirana Wenye Ulemavu Mhe. Jenister Mhagama amesema sekta ya hifadhi ya jamii inachangia pato la Taifa kwa asilimia 10, na kwamba imedhamiria kupanua uwigo wake wa kuchangia katika nguvu kazi ya Taifa kutoka asilimia 11 hadi kufikia asilimia 40 ifikapo mwaka 2025.

Wabunge wa Mkoa wa Morogoro wamemshukuru Mhe. Rais Magufuli kwa miradi mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa katika majimbo yao ikiwemo ujenzi wa barabara, zahanati, vituo vya afya na hospitali, elimu na ujenzi wa viwanda, na wamemuomba awasaidie kushughulikia matatizo ya ufujaji wa fedha za miradi ya maji na ujenzi wa barabara, kutatua tatizo la maji katika Manispaa ya Morogoro na kusuasua kwa ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Mkunazi.

Mhe. Rais Magufuli amewapongeza wananchi wa Morogoro kwa kupata kituo cha mabasi cha kisasa na ameahidi kuwa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuiwezesha Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kuchukua hisa zote za kituo hicho kutoka LAPF ili kiwe chini ya umilikiwa wake kwa asilimia 100.

Aidha, Mhe. Rais Magufuli ameagiza wafanyabiashara wadogo (*Wamachinga*), Mama na Baba Lishe na Bodaboda wasizuiwe kuuza bidhaa zao na kutumia kituo hicho, na ameiagiza Wizara ya TAMISEMI kuhakikisha vituo vyote vya mabasi vinavyojengwa nchi nzima vinazingatia uwepo wa maeneo ya Wamachinga, Mama na Baba Lishe pamoja na Bodaboda.

***“Siwezi kufungua kituo cha mabasi ambacho kina ubaguzi, nilichaguliwa na watu wote wakiwemo wamachinga, Mama lishe, Baba Lishe na waendesha Bodaboda, nataka hawa nao wanufaike na kituo hiki, na nakuagiza Waziri hakikisha kote ambako vituo vya mabasi vinajengwa hawa nao wanatengewa sehemu za kufanyia shughuli zao”*** amesisitiza Mhe. Rais Magufuli.

Kuhusu ufujaji uliodaiwa kufanywa katika ujenzi wa barabara ya Tubuyu - Nanenane Mhe. Rais Magufuli amemuagiza Waziri wa TAMISEMI kufuatilia na kuchukua hatua stahili, na pia ameahidi kufuatilia na kuzifanyia kazi kero nyingine zilizotolewa na Wabunge wa Morogoro.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, IKULU  
Morogoro  
06 Mei, 2018